HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU

MUHTASARI WA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 23-24/02/2017.

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. Juma A. Kimisha - Diwani Kata ya Nyamilangano- **Mwenyekiti**
2. Mhe. Gagi Lala Gagi - Diwani Kata ya Igwamanoni – **Makamu Mwenyekiti**
3. Mhe. Elias J. Kwandikwa - Mbunge Jimbo la Ushetu
4. Mhe. Tabu R. Katoto - Diwani Kata ya Igunda
5. Mhe. Yohana E. Mange - Diwani Kata ya Mapamba
6. Mhe. Emmanuel N. Makashi - Diwani Kata ya Sabasabini
7. Mhe. Mabala K. Mlolwa - Diwani Kata ya Chona
8. Mhe. Yuda L. Majonjos - Diwani Kata ya Idahina
9. Mhe. Mkomba P. Daudi - Diwani Kata ya Ukune
10. Mhe. Kulwa D. Shoto - Diwani Kata ya Bukomela
11. Mhe. Bundala J. Christopher - Diwani Kata ya Uyogo
12. Mhe. Benedicto A. Mabuga - Diwani Kata ya Mpunze
13. Mhe. Pili E. Sonje - Diwani Kata ya Ushetu
14. Mhe. Sharifu A. Samwel - Diwani Kata ya Kinamapula
15. Mhe. Paschal N. Mayengo - Diwani Kata ya Ulowa
16. Mhe. Doa M. Limbu - Diwani Kata ya Nyankende
17. Mhe. Kulwa E. Mabula - Diwani Kata ya Ulewe
18. Mhe. Damas J. Njige - Diwani Kata ya Chambo
19. Mhe. Hamis M. Majogoro - Diwani Kata ya Ubagwe
20. Mhe. Joseph M. Masaluta - Diwani Kata ya Bulungwa
21. Mhe. Golani P. Sayi - Diwani Kata ya Kisuke
22. Mhe. Bernadetha M.Jumanne - Diwani Viti Maalum
23. Mhe. Mary I. Lundalila - Diwani Viti Maalum
24. Mhe. Bether L. Bugaywa - Diwani Viti Maalum
25. Mhe. Esther M. Imambo - Diwani Viti Maalum
26. Mhe. Felister N. Kabasa - Diwani Viti Maalum
27. Mhe. Eva P. Mkonya - Diwani Viti Maalum
28. Mhe. Gabriela A. Kimaro - Diwani Viti Maalum

WATAALAM WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Sadick J. Mwita . - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) **- Katibu**
2. Ndg. Anna Ngongi - Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)

3. Ndg. Suzan kiunsi - Mhasibu
4. Ndg. Manyama Katikiro - Afisa Utumishi (W)
5. Ndg. Edith Mpinzile - Afisa Elimu Msingi (W)
7. Ndg. Gervas Magogozwa - Afisa Utamaduni (W)
8. Ndg. John Duttu - Kaimu Mganga Mkuu (W)
9. Ndg. Deus Kakulima - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
10. Ndg. Nyalali Ndaki - Kaimu Mhandisi wa Maji (W)
11. Ndg. John Kabisi - Mhasibu
12. Ndg. Onesmo Benjamin - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
13. Ndg. Melkiad Gaka - Afisa Elimu Sekondari (W)
14. Ndg. Elisha Mahungo - Mratibu wa TASAF III
15. Ndg. Dismas B. Karenga - Kny: Afisa Ushirika
16. Ndg. Neuster James - Mwanasheria (W)
17. Ndg. Marco Mwairwa - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
18. Ndg. Mogan Mwita - Mratibu wa kudhibiti UKIMWI
19. Ndg. Goodkuck Ndunguru - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
20. Ndg. Valentina C.Majembe - Afisa Utumishi - TSC
21. Ndg. Victor Mhapa - Kaimu Afisa Uchaguzi (W)
22. Ndg. Elly Nkiko - Mhasibu Mapato
23. Ndg. Juma R. Ngogo - Afisa Mipango Miji
24. Ndg. Selestine Lufundisha - Afisa Biashara
25. Ndg. Aston Mnkeni - Kny: Mkaguzi wa Ndani (W)
26. Ndg. Elnight Mmari - kaimu Afisa Ugavi (W)
27. Ndg. Cosmas Maganga - Mhasibu TASAF
28. Ndg. Abeid M.Meza - Mthibiti Mkuu wa Ubora wa Shule (W) Kahama
29. Ndg. Athanas Lucas - Afisa Usafi na Mazingira (W)
30. Ndg. Benedicto Anthony - Kaimu Mweka Hazina (W)
31. Ndg. Tumshukuru C.Mdui - Afisa Tarafa - Dakama
32. Ndg. Salakana J. Peter - Afisa Tarafa – Mweli
33. Eng. Bright Mndeme - Mhandisi wa Ujenzi (W)
33. Ndg. Bahati Rashid - Mhasibu

WAGENI WAALIKWA WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Frenk Elophazy - Mkuu wa kikosi cha zimamoto
2. Ndg. Alphonce S. Kasanyi - Kny: Katibu Tawala (M) Shinyanga
3. ASP. Alphonce Bandya - Afisa Upelelezi Kituo cha Polisi Nyamilangano
4. Ndg. Mtua Hassan - kny: Afisa Usalama (W)
5. Ndg. Emmanuel Battemi - Dereva Uhamiaji
6. Ndg. Alexandrina M. Katabi - Katibu wa Chama cha Mapinduzi (W).
7. Ndg. Mkolla A. Kabali - Katibu UVCCM (W)

8. Ndg. Henry Mwala - Afisa Uhamiaji
9. Ndg. Lusana Shigumha - Kny: Mkuu wa Magereza
10. Ndg. Frednand Julius - Mshauri wa Mgambo (W)
11. Ndg.Julius Lugobi - Katibu Ofisi ya Mbunge Jimbo la Ushetu
12. Ndg.Salvatory Cevin - Mwandishi wa Habari – Kahama FM
13. Ndg.Nyamitti A. Nyamitti - Mwandishi wa Habari – Divine FM
14. Ndg.Simon Dionizy - Mwandishi wa Habari – Kwizera FM
15. Ndg. Shaban Njia - Mwandishi wa Habari – Jamboleo
16. Ndg. Ali Lityawi - Mwandishi wa Habari – Tanzania Daima
17. Ndg. Patrick Mabula - Mwandishi wa Habari – Majira
18.Michael francis Bundala - Mwandishi wa Habari – Baloha FM

SEKRETARIETI

1. Ndg. Chamo Mashauri - Mwandishi wa Vikao (CC)
2. Ndg. Warda Yusuph - Mwandisha wa Vikao (CC)

MUHT.NA.BM/40/2016/2017 - KUFUNGUA MKUTANO

Katibu aliwakaribisha wajumbe, wageni waalikwa na wataalam katika kikao na kisha kumkaribisha mwenyekiti kufungua kikao

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe, wageni waalikwa na wataalam katika kikao na kueleza kuwa kikao hicho ni Baraza la kawaida na kwa mujibu wa akidi imetimia hivyo kikao ni halali kufunguliwa pia alisema kuwa kikao hicho agenda zimeorodheshwa kwenye kabrasha hivyo wajumbe watakapojadili wajikite moja kwa moja kwenye agenda.

Aidha alisema kuwa Halmashauri ya Ushetu imebeba eneo kubwa la wilaya ya Kahama hivyo inahitaji nguvu kubwa katika kuwahudumia wananchi.

Alifungua kikao saa 05:05 asubuhi.

MUHT.NA.BM/41/2016/2017 – KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO

Wajumbe waliridhia kujadili agenda kumi na moja (11) kama ifuatavyo:

Tarehe 23/02/2017

1. Kufungua mkutano
2. Kuridhia agenda za mkutano
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 16-17/11/2016
4. Yatokanayo na Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 16-17/11/2016
5. Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi kinachoishia mwezi Desemba, 2016

6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ngazi ya kata
7. Kusitisha mkutano wa Baraza

Tarehe 24/02/2017

8. Kurejea kwa mkutano wa Baraza
9. Maswali ya papo kwa papo
10. Taarifa za Kamati za kudumu za utekelezaji wa shughuli za Halmashauri katika kipindi cha robo ya pili Oktoba - Desemba, 2016
    a) Kamati ya kudhibiti UKIMWI
    b) Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira
    c) Kamati ya Elimu, Afya na Maji
    d) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango
11. Kufunga mkutano

MUHT.NA.BM/42/2016/2017 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI

Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari wa Mkutano wa kawaida wa Baraza la Madiwani tarehe 16-17/11/2016 ukurasa kwa ukurasa.

Baada ya kupitia muhtasari, wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo ni sahihi hivyo Katibu na Mwenyekiti walisaini kwa ajili ya kumbukumbu halali za Halmashauri.

MUHT.NA.BM/43/2016/2017 – YATOKANAYO NA MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 16-17/11/2016

Majibu ya utekelezaji wa yatokanayo yaliwasilishwa kama ifuatavyo:

Kutoka Muht. Na. BM/20/ 2016/2017- Kuhusu ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri

Iliazimiwa kuwa ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri ufanyike Januari 2017 kama mapendekezo yalivyowasilishwa na kuridhiwa kupitia vikao vya kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na Baraza la madiwani.

Utekelezaji, matangazo yamekwisha tolewa timu ya tathimini iliketi na kufanya tathimini ambapo wazabuni walioshinda wataanza kazi ya ukusanyaji mwezi Fubruari,2017 kutokana na mchakato wa manunuzi mkataba utakamilika mwezi Februari.

Mhe. Esther M. Imambo alishauri maeneo ya ukusanyaji wa mapato yabinafsishwe kutokana na mapato mengi kupotea kupitia njia ambazo si sahihi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuhusu ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato kuwa kuna wazabuni waliokuwa wameomba zabuni lakini kiasi cha fedha kilikuwa kiko

chini hivyo aliomba Baraza kama litaridhia wazabuni waitwe ili kufanya makubaliano na kuelekezwa Halmashauri inahitaji kufikia kiasi gani cha fedha katika vyanzo hivyo walivyoomba na kama watakubali ndipo mkataba usainiwe.

Baada ya kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) kutoa ombi hilo wajumbe waliunga mkono rai hiyo na kueleza kwamba wazabuni waongeze gharama kwenye vyanzo ambavyo viko chini kisha wapewe zabuni.

Kutoka Muht. Na. BM/20/2016/2017 – kuhusu kitabu cha kukusanyia mapato kilichopotea katika kizuizi/geti la Mpunze

Iliazimiwa kwamba Mkurugenzi Mtendaji aendelee kuikumbusha polisi kufanya upelelezi wa suala hilo na kukamillisha mapema iwezekanavyo (hadi siku ya kikao, upelelezi ulikuwa haujakamilika ili hatua zaidi zichukuliwe)

Mambo muhimu:

i) Ni kwa namna gani kitabu kile kilipotea.

ii) Ni kiasi gani cha fedha kilikuwa kimekusanywa kpitia kitabu hicho na zitawasilishwaje kwa Halmashauri.
Fedha iliyokuwa imekusanywa kupitia kitabu hicho irejeshwe na hatua za kisheria zichukuliwa kwa wote waliosababisha upotevu huo.

Utekelezaji, uchunguzi wa polisi bado unaendelea.

Baada ya majibu ya azimio hilo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Emmanuel N. Makashi alitaka kujua ni kwa nini uchunguzi wa kipolisi unachelewa ili hali mtumishi tayari anaonekana anamakosa ni kwa nini asipishe uchunguzi. Aidha aliomba polisi wapewe ushirikiano ili kuweze kufanikisha uchunguzi jambo hilo.

Mhe. Paschal N. Mayengo alieleza kuwa kila sehemu inautaratibu wake polisi wanautaratibu wao na bado wanaendelea na uchunguzi lakini upande wa ofisi kuna kikwazo kipi kinachopelekea mtumishi huyu kushindwa kusimamishwa ili apishe uchunguzi aliomba maeneo ambayo yanahitaji kutoa ushirikiano kwa polisi wataalamu watoe ushirikiano na mamlaka za kinidhamu zichukue hatua katika eneo ambalo mtumishi huyo anafanyia kazi.

Mwenyekiti aliagiza kuwa mtumishi aliyekuwa anasimamia geti la mpunze asimamishwe kazi kupisha uchunguzi ili mamlaka iendelee kufanya utafiti. Aidha Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iendelee kufuatilia na kutoa ushirikiano kwa polisi ili kuweza kumaliza suala la upotevu wa kitabu.

Kutoka Muht. Na BM/21/2016/2017 – kuhusu utumikaji wa stakabadhi za kuandikwa kwa mkono

Iliazimiwa kuwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ifuatilie kujua mashine za kukusanyia mapato kielektroniki zimeshaletwa na vitabu vikaondolewa kwanini baadhi ya mageti kama Mpunze bado wanaendelea kutumia stakabadhi na kuandika kwa mkono.

Utekelezaji, mashine za kielektroniki zilikuwa 10 tu ambazo hazitoshi kwa mahitaji ya Halmashauri, hii ni pamoja na shida ya mtandao kwa maeneo mbalimbali ya Halmashauri kwa mantiki hiyo stakabadhi za mkono ziliendelea kutumika.

Baada ya majibu ya azimio hilo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Emmanuel N. Makashi alieleza kuwa kuwepo kwa mashine kuna faida nyingi ikiwa ni pamoja na kuonesha taarifa mbalimbali za ukusanyaji wa mapato na kuweza kujua ni kiasi gani kilikusanywa ikiwa ni pamoja na kutunza kumbukumbu.

Mwenyekiti alieleza kuwa ukusanyaji wa mapato kwa kupitia mashine ilikuwa ni agizo la serikali.

Kutoka Muht. Na. BM/23/2016/2017 – kuhusu walezi wa kata

Ilielezwa kuwa Kamati Tendaji (CMT) iwajibike katika kuandaa walezi wa kila kata na wajulikane katani na wafanye kazi yao.

Utekelezaji, orodha hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Nyamilangano - C. Akyoo (DHRO)
2. Mapamba - A. Ngongi (DAICO)
3. Igwamanoni - O. Benjamin (DCDO)
4. Ulowa - K.H. Licas (DBO)
5. Mpunze - S. Lufundisha (DTO)
6. Sabasabini - M. Mwairwa (DLNRO)
7. Igunda - A. Lucas (DEHSO)
8. Chona - D. Kakulima (DFLO)
9. Bulungwa - J. Wanyancha (HICT)
10. Bukomela - S. Nyeriga (DT)
11. Uyogo - M. Gaka (DSEO)
12. Ubagwe - E. Mpinzile (DPEO)
13. Ukune - B. Mndeme (DE)
14. Kinamapula - S.J. Mwita (HPMU)
15. Idahina - J. Mpira (AG. DEO)
16. Ushetu - J. Duttu (AG. DMO)
17. Nyankende - F. Mallya (DPLO)
18. Chambo - N. James (DLO)
19. Kisuke - C. Pambe (DWE)

20. Ulewe - P. Karol (DIA)

Baada ya majibu ya azimio hilo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Damas J. Njige alishauri walezi wa kata watekeleze wajibu wao katika kata husika walizopangiwa na si majina hayo kuishia kwenye kablasha.

Rai hiyo iliungwa mkono na Mhe. Emmanuel N. Makashi na kupongeza uteuzi wa walezi wa kata na aliongeza kuwa uteuzi huo utapunguza migogoro katika kata.

Kutoka Muht. Na. BM/23/2016/2017 – kuhusu kanuni za kudumu za Halmashauri
Ilielezwa kuwa kuhakikisha kanuni za kudumu za Halmashauri ya Ushetu zinafuatiliwa ili zisainiwe na mamlaka husika tayari kwa matumizi

Katika utekelezaji wake majibu hayakuwekwa. Baada ya azimio hilo kuwasilishwa,wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Paschal N. Mayengo alishauri kwa kuwa taarifa zinazokuwa katika kablasha ni kumbukumbu halali za Halmashauri ya Ushetu ni vyema zisiwe zinaachwa wazi bila kujazwa angalau iandikwe majibu bado yanafuatiliwa.

Mhe. Felister N. Kabasa alitaka kujua ni kwa nini majibu ya utekelezaji hayakujazwa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa majibu yalikuwa bado hayajapatikana kutokana na mawasiliano ya ofisi ya sheria TAMISEMI kuwa bado haijatoa majibu lakini hadi kufikia tarehe ya kikao tayari mawasiliano yalifanyika na majibu yalishatolewa na kanuni hizo za Halmashauri ziko mezani kwa Waziri mwenye Dhamana.

Mhe. Elias J. Kwandikwa (MB) alishauri kuwa kwa masuala yote yanayohusu ofisi za TAMISEMI ashirikishwe katika kufuatilia kwani mara nyingi anakuwa katika ofisi hizo hivyo anaweza kufuatilia jambo lolote kwa karibu zaidi.

Kutoka Muht. Na. BM/27/2016/2017 – kuhusu kupangisha majengo ya Halmashauri ya wilaya ya Ushetu yaliyopo mjini Kahama

Iliagizwa kuwa Halmashauri ya wilaya ya Ushetu iligawana rasilimali na Halmashauri ya wilaya ya Msalala na si vinginevyo na kwamba majengo yaliyopo mjini Kahama ni mali halali ya Halmashauri ya Ushetu na wananchi wake, Mkurugenzi Mtendaji (W) Ushetu aanze mara moja mchakato wa kupangisha majengo hayo kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri.

Utekelezaji, matangazo ya ubinafsishaji huo hayakufanyika kutoka na ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kupokea barua kutoka kwa Katibu Tawala (M) yenye kumbu. Na. CAB.

3/290/02/ “A”/5 ya tarehe 01/12/2016 ikielekeza kukabidhi majengo hayo kwa Halmashauri ya Kahama Mji.

Baada ya majibu ya azimio hilo kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Elias J. Kwandikwa alishauri kuwa Halmashauri ya Ushetu ifanye uwekezaji kama kampuni hivyo wataalam wanatakiwa kuandaa mpango wa kitaalam unaoonesha/elekeza jinsi ya kuandaa uwekezaji huo.

Mhe. Pili E. Sonje aliipongeza kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa ufuatiliaji waliofanya wa majengo ya Halmashauri ya Ushetu yaliyopo mjini Kahama na kuongeza kuwa katika majengo yale uwekezaji uendelee kufanyika hivyo azimio la uwekezaji katika majengo yaliyopo mjini Kahama liendelee.

Aidha aliomba baadhi ya vyumba vibakizwe kwa ajili ya wataalamu kuendelea kufanya kazi katika majengo hayo. Pia ofisi hizo ziendelee kutunzwa kama ilivyokuwa zamani/awali, zifanyiwe ukarabati na kuwekewa bango linaloonesha kuwa Ofisi zile ni za Halmashauri ya Ushetu, Vifaa vya ofisi vilivyopo Nyamilangano ambavyo vimekosa mahala pa kuwekwa vikatunzwe katika majengo yaliyopo mjini Kahama, maji yarudishwe, kuwe na umeme, ufanyike usafi na iwekwe bendera kwa sababu majengo hayo ni ya serikali.

MUHT.NA.BM/44/2016/2017 – TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI KINACHOISHIA MWEZI DESEMBA, 2016

Kaimu Mweka Hazina (W) aliwasilisha taarifa hiyo na kusema kuwa kwa kipindi cha mwezi Desemba, 2016 Halmashauri ilikusanya na kupokea sh. 2,795,587,551.62 na kutumia jumla ya sh.1,492,681,220,05 kutoka vyanzo vya ndani na Serikali Kuu kama ifuatavyo:

A	MAPATO	Makisio ya mwaka 2016/2017 Sh.	Mwezi Desemba 2016/2017 sh.	Julai – Desemba 2016/2017 Sh.	Albaki sh.	%
	Mapato ya Ndani	2,317,292,200	87,444,750.00	1,266,518,979.54	1,050,773,220.46	55
	Ruzuku za idara OC & GPG	1,345,466,000	21,659,000.00	311,672,000.00	1,033,794,000.00	23
	Mishahara (PE)	15,055,791,000	1,254,649,249.30	7,528,832,840.30	7,526,958,159.70	50
	Miradi ya Maendeleo	8,105,585,042	740,043,244.32	1,594,630,365.05	6,510,954,676.95	20
	Jumla	26,824,134,242	1,432,634,552.32	3,027,264,917.37	5,078,320,124.63	37
B	**MATUMIZI**					

	Matumizi ya kawaida (Mapato ya Ndani)	822,720,880	78,588,473.75	495,530,429.07	405,778,924.68	60
	Ruzuku za idara (OC) & GPG	1,345,466,000	25,689,000.00	288,538,474.00	1,056,927,526.00	21
	Mishahara (PE)	15,055,791,000	1,254,649,249.30	7,539,863,616.80	7,515,927,383.20	50
	Mikopo ya Wanawake na Vijana (10%)	150,320,000	-	31,500,000.00	118,820,000.00	21
	Matumizi ya Miradi ya maendeleo (Mapato ya ndani)	1,083,761,320	39,026,179.80	264,055,585.91	819,705,734.09	24
	CHF, NHIF &Papo kwa papo	260,490,000	-	2,058,335.47	260,490,000.00	0
	Fedha toka serikali kuu & wafadhili	8,105,585,042	94,728,317.20	1,751,423,900.24	6,354,161,141.76	22
	Jumla kuu	26,824,134,242	1,492,681,220.05	10,114,382,599.9	16,709,751,642.09	38

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Kulwa D. Shoto alieleza kuwa uhai wa Halmashauri ni mapato na tayari katika kipindi cha robo ya pili Halmashauri ya Ushetu imefanikiwa kukusanya nusu ya malengo iliyojiwekea kwa mwaka mzima. Aidha aliongeza kuwa Ruzuku ya serikali ni asilimia 23 na mishahara ni 50% hivyo serikari inafanya kazi vizuri kwa kuangalia wananchi wake. Alimpongeza Mhe. John Pombe Magufuli Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya kazi vizuri na kuweza kuleta ruzuku katika Halmashauri.

Mhe. Eva P. Mkonya alitoa ushauri kwa Idara ya Ardhi na Maliasili kuwa ni vyema Idara hiyo ikaanza upimaji wa viwanja/maeneo ili kuweza kuongeza mapato na hasa ukizingatia kiwango cha ukusanyaji wa mapato katika idara hiyo kiko chini zaidi.

MUHT.NA.BM/45/2016/2017 – TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI NGAZI YA KATA

Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Kata za Ushetu, Sabasabini, Kinamapula, Chambo, Ukune, Kisuke, Igwamanoni, Ulewe, Nyamilangano na Bulungwa ziliwasilishwa na madiwani wa Kata husika.

Baada ya taarifa hizo kuwasilishwa Mhe. Elias J. Kwandikwa (Mb) aliwapongeza waheshimiwa Madiwani katika kuwasilisha taarifa zao aliongeza kuwa katika ushirikishwaji amefurahishwa na suala la madiwani wa viti maalum kushirikishwa na kuwasilisha taarifa za baadhi ya kata. Pia alisema suala la uwazi, uwajibikaji na nidhamu kwa upande wa waheshimiwa madiwani liko vizuri.

MUHT.NA.BM/46/2016/2017 – KUSITISHA MKUTANO WA BARAZA

Msaidizi wa katibu tawala serikali za mitaa (M) alimpongeza Mhe. Elias J. Kwandikwa (MB) kwa kusema kuwa Ushetu imepata faida kutokana na kuwa na mbunge makini anaefuatilia masuala ya Halmashauri ya Ushetu.

Aidha aliongea kuhusu suala la ulinzi na usalama na kueleza kuwa kumekuwa na tabia za watu wasio na nia njema na wananchi wanawavamia kwa kutumia silaha za moto na kuwauwa. Hivyo alipongeza Halmashauri ya Ushetu kwa kuwa na kituo cha polisi na kumpata kamanda ambae ni Afisa upelelezi kituo cha polisi Nyamilangano ASP. Alphonce Bandya hivyo alimkaribisha na kuomba kufanya kazi kwa kushirikiana na wananchi.

Pia aliongea Kuhusu taarifa za utekelezaji ngazi za kata kuwa uwasilishwaji unafanyika vizuri kwani inaonesha wazi ushirikishwaji wa wananchi kuanzia ngazi za vijiji na suala hili la ushirikishwaji ni sera ya serikali.

Baada ya Afisa serikali za mitaa kuwasilisha aliyokuwa nayo katibu alimkaribisha mwenyekiti kusitisha kikao.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki vizuri katika agenda zilizowasilishwa na kujadiliwa. Alieleza kuwa Halmashauri itaendelea kusimamia kanuni na taratibu na hasa katika kupigania mali za wananchi. Aidha alieleza kuwa hatarajii kuendesha vikao kwa ugumu kwa ajili ya maazimio yanayokuwa yametolewa na waheshimiwa madiwani kwa kutokutekeleza. Alisema kuwa Halmashauri itaendeleea kufanya kazi kwa kushirikiana ili kutekeleza yale yote ambayo yatakuwa na manufaa kwa wananchi wake.

Alisitisha Mkutano saa 07:30 mchana.

MUHT.NA.BM/47/2016/2017 – KUREJEA KWA MKUTANO WA BARAZA TAREHE 24/02/2017

Katibu aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kisha kumkaribisha mwenyeki kurejesha kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao na kueleza kuwa mkutano huo ni mwendelezo wa mkutano wa baraza la kawaida ambao unafanyika kwa siku mbili. Na baada ya kusema hayo alirejesha mkutano saa 10:45 asubuhi.

MUHT.NA.BM/48/2016/2017 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO

Mwenyekiti alieleza kuwa hadi Mkutano huo unaanza, alikuwa hajapokea swali lolote la papo kwa papo hivyo aliruhusu agenda nyingine ziendelee.

MUHT.NA.BM/49/2016/2017 – TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA PILI OKTOBA - DESEMBA, 2016

Taarifa hizo ziliwasilishwa na wenyeviti wa kamati husika kama ifuatavyo:

A. KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.Gagi Lala Gagi aliwasilisha taarifa ya kamati yake alieleza kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, katika kipindi cha robo ya pili, Halmashauri kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa huduma za kukabiliana na VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI, huduma za wagonjwa majumbani, ushauri nasaha na upimaji VVU kwa hiari na huduma ya bure ya dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Juhudi hizi zililenga kufikia malengo ya sifuri tatu **"Maambukizi Mapya Sifuri, Unyanyapaa na Ubaguzi Sifuri na Vifo vitokanavyo na UKIMWI sifuri.**

Matumizi ya fedha za kudhibiti VVU NA UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati hiyo aliendelea kueleza kuwa Halmashauri ilipanga kutekeleza shughuli 9 kwa kutumia fedha za Mwitikio wa Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI (NMSF) kwa gharama ya Tshs 18,501,024 na shughuli 4 kwa kutumia fedha za mapato ya ndani kwa gharama ya Tshs 5,018,750 na kufanya jumla ya Tshs 23,519,774 zilizotarajiwa kutumika.

Kitengo kilifanikiwa kutekeleza shughuli 8 kwa kutumia fedha za NMSF kwa gharama ya Tshs 15,828,686.

Huduma za tiba na matunzo (CTC)

Ilielezwa kuwa huduma hiyo ilitolewa katika vituo 11 vya tiba na matunzo ambapo jumla ya watu 496 walijiandikisha CTC kuanzia Oktoba - Desemba 2016 ambapo watu 715 wameshaanza huduma ya dawa.

Changamoto za kukabiliana na VVU/UKIMWI

1. Uwepo wa uhitaji mkubwa wa misaada kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI
2. Uwepo wa maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI
3. Baadhi ya watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kukatiza matumizi ya dawa.

Mikakati ya kukabiliana na changamoto

1. Kutafuta wadau (Asasi) wa kusaidia katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI
2. Kuimarisha kamati za kudhibiti UKIMWI za vijiji na kata kusaidia katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI
3. Kuendelea kushirikiana na watoa huduma majumbani kuwatafuta waliokatiza matumizi ya dawa.

Baada ya mwenyekiti kuwasilisha taarifa ya kamati ya kudhibiti ukimwi
wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

Mhe. Paschal N. Mayengo alieleza kuwa chumba cha ugawaji wa dawa CTC katika zahanati ya Ulowa ni kidogo ambapo chumba hicho kinatumika kutolea dawa kwa wagonjwa wengine wa kawaida na hivyo haimpi uhuru mgonjwa anayeenda kupata huduma katika chumba cha CTC hivyo alitaka kujua ni lini chumba cha kutolea huduma ya CTC kitapanuliwa.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa suala hilo litatekelezwa kutokana na mpango wa bajeti.

Mhe. Paschal N. Mayengo alishauri kuwa suala la changamoto ya CTC Zahanati ya Ulowa lichukuliwe na litekelezwe kama suala la dharula kwani kuendelea kusubili ni kufanya wagonjwa kutokupata huduma kituoni hapo.

Mhe. Hamis M. Majogoro alishauri kuwa Halmashauri iweke mpango mahususi wa kuchimba mabwawa na kufuga samaki,alieleza kuwa ufugaji huo unasaidia upatikanaji wa samaki hivyo kuboresha lishe na upatikanaji wa maji katika shughuli anuwai.

Mwenyekiti alieleza kuwa uchimbaji wa mabwawa hutokana na mpango wa bajeti. Hata hivyo watu binafsi na vikundi wanaweza kupata elimu ya ufugaji wa samaki kutoka kwa wataalamu ili kuboresha afya zao na kuinua uchumi.

Mhe. Sharifu A. Samwel alieleza kuwa kamati ya kudhibiti UKIMWI ilitembelea kata ya kinamapula kuona mabwawa ya samaki alitaka kujua Idara ya Mifugo na Uvuvi imejipangaje kuweza kuwasaidia wananchi waweze kupata vifaa vya kuvunia samaki, uchimbaji wa mabwawa na kuweza kusambaza elimu ya kutosha juu ya uvunaji wa samaki.

Afisa mifugo na Uvuvi (W) alieleza kuwa wafugaji wa samaki wajitahidi kununua vifaa vinavyowawezesha kuvua samaki kwani hiyo ni shughuli binafsi. Halimashauri inaweza kupeleka msaada pale mabwawa hayo yanapokuwa yamemilikiwa na taasisi ya umma au kikundi.

A. KAMATI YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.Tabu R. Katoto aliwasilisha taarifa ya kamati yake, taarifa ya kamati yake ilihusisha masuala yafuatayo:

Kuhusu utengenezaji wabarabara kwa kutumia mitambo ya Halmashauri

Ilielezwa kuwa zitengwe Fedha kama ilivyo kwenye mpango wa bajeti shilingi milioni 90 kwa ajili ya matengenezo ya barabara km 20 kila kata na ukarabati uanze mara moja.

Kuhusu kilimo cha Alzeti

Ilielezwa kuwa barua yenye kumb. Na.A/20/7/220 ya tarehe 22/12/2016 iliandikwa kwa watendaji wa Kata na Vijiji na kuwaelekeza kushirikiana na maafisa ugani waliopo katika ngazi ya kata kuhamasisha ununuzi wa mbegu na kilimo cha alzeti.

Taarifa ya uendeshaji mitambo ya Halmashauri

Ilielezwa kuwa mapato ya mitambo kuanzia kipindi cha Oktoba – Desemba, 2016 ni makusanyo ya mitambo yote mpaka kufikia tarehe 31/12/2016, kiasi cha Tsh. 25,200,000.00 zilikusanywa kwa kukodishwa *grader, roller na lowbed* kwa kazi mbalimbali za wakandarsi. Pia kilometa 12 za barabara za Halmashauri ya Ushetu zilichongwa katika kipindi cha mwenge sawa na thamani ya Tsh. 4,000,000.00 na kiasi cha Tsh. 3,000,000.00 za *Lowbed* kwa ajili ya kuhamisha mitambo kama *Grader na Roller* hivyo jumla ya Tsh. 7,000,000.00 zingeweza kutumika kama ingekodishwa. Barabara zilizochongwa wakati wa mwenge kipindi hicho ni katika maeneo ya Nshimba, Mapamba, Nyamilangano, Sabasabini na Bulungwa.

Pia Halmashauri imeweza kuingia mkataba na kampuni ya Tingwa Co. Ltd kwa kutengeneza barabara katika maeneo yaliyohatarini kujifunga kwa barabara katika maeneo ya Bugomba A darajani, Bugomba A njia panda, Ubagwe na Ulowa darajani kwa thamani ya Tsh. 30,500,000.00 kiasi ambacho kama kazi hii ingefanywa na mkandarasi, Halmashauri ingetumia Tsh. 52,850,500.00 kulipa kazi hizo.

Makusanyo haya yanafanya jumla ya kiasi chote kilichotakiwa kukusanywa ikiwa ni pamoja na shughuli za Halmashauri kuwa Tsh. 62,700,000.00 yakiwa ni malipo nje ya shughuli zilizofanywa na Low bed kwa kusambaza madawati katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri yetu.

Ilielezwa kuwa gharama za ukodishaji wa mitambo ya Halmashauri ni shs. 1,000,000.00 kwa *grader* kwa masaa 8 ya kazi kwa siku na shs. 500,000.00 kwa *roller* kwa masaa 8 ya kazi kwa siku.

Taarifa ya uhitaji wa uboreshaji wa miundo mbinu minadani

Ilielezwa kuwa biashara ya mifugo nchini huendeshwa kwa kuzingatia sheria zifuatazo:-

- Sheria ya magonjwa ya wanyama Na. 17 ya mwaka 2003

- Sheria ya nyama Na. 10 ya mwaka 2006
- Sheria ya biashara ya ngozi Na. 18 ya mwaka 2008
- Sheria ya ustawi wa wanyama Na. 19 ya mwaka 2008
- Sheria ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 na
- Sheria ya leseni za biashara Na. 25 ya mwaka 1972 na marekebisho yake ya mwaka 1980.

Kwa matakwa ya sheria Na. 10 ya mwaka 2006, kanuni ya uendeshaji wa masoko ya mifugo kifungu Na. 5 (1-3) mnada wa mifugo unatakiwa uwe na miundo mbinu ifuatayo:-

- Sehemu ya kushusha na kupakia mifugo
- Kiringe cha kunadia mifugo chenye mizani
- Mazizi ya mifugo inayouzwa, iliyonunuliwa na mifugo iliyotengwa kwa sababu mbalimbali
- Maji na eneo la kuchungia
- Uzio kuzunguka eneo la mnada
- Ofisi na vyoo
- Shimo au tanuru la uchafu.

Kwamba Waraka wa matumizi ya mizani katika biashara ya mifugo wa mwaka 2010 ulioandikwa na aliye kuwa waziri wa Mifugo na Uvuvi Mh. Dr. John Pombe Magufuri unasisitiza matumizi ya mizani minadani kwa lengo la kumwezesha mfugaji kupata malipo sahihi kulingana na thamani ya mifugo yake, kuleta uwazi na ushindani katika biashara ya mifugo na kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi za biashara ya mifugo zinazo wiana kitaifa kwa madaraja, uzito na ubora.

Ilielezwa kuwa katika maelekezo kupitia mkutano uliofanyika mjini Dodoma tarehe 28/01/2017 umeagiza kufanya yafuatayo:-

- Mifugo yote wauzwe kwa mizani hivyo kila mnada-uwe na mzani ndani ya kiringe cha kupimia mifugo.
- Kila mnada uwe na uzio ili kudhibiti upotevu wa mapato na wachuuzi kati.
- Kila mnada uwe na kibali cha waziri mwenye dhamana au mkaguzi awe ametoa kibali cha muda wa matazamio wakati harakati za kupata kibali toka kwa waziri mwenye dhamana zinaendelea.
- Kila mnada utengwe (partition) kadiri ya mahitaji ya mifugo.
- Minada ambayo haijakidhi vigezo ifungwe kabla ya ukaguzi wa kitaifa kufanyika.

Ilipendekezwa kwa kuanzia Halmashauri inusuru minada mitatu (3) ya Chona, Uyogo na Bugomba kwa kuijengea uwezo wa miundo mbinu kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi, vinginevyo minada hiyo ifungwe rasmi ndani ya mwezi mmoja kama maagizo yalivyotolewa .

Idara ya Ardhi na Maliasili

Ilielezwa kuwa katika upande wa Mipango Miji idara ilipanga kufanya upimaji katika miji midogo minne ambayo ni Nyamilangano, Mseki (Bulungwa), Mbika (Ushetu) na Kangeme

(Ulowa) lakini mji wa kangeme haujaoneshwa katika mpango wa kuandaa michoro ya mipango miji katika Halmashauri hivyo ilielezwa Kangeme (Ulowa) irejeshwe kwenye mpango na upimaji ufanyike. Iliongezwa kuwa kazi ya kuandaa michoro kwa ajili ya upimaji wa miji midogo iliyokuwa imepangwa kupimwa imefanyika kwa muda mrefu hivyo ni wakati wa kuanza kufanya utekelezaji kuepusha ujenzi holela unaoendelea kufanyika.

Ilielezwa kuwa hadi kufikia robo ya pili Oktoba Desemba, 2016 idadi ya viwanja vilivyokuwa vimepimwa ni viwanja 340, kuhusiana na mji wa Kangeme (Ulowa) ilielezwa kuwa ni tatizo la uchapaji mji huo upo katika mpango na utaendelea kuonekana katika mpango wa upimaji.

Baada ya mwenyekiti kuwasilisha taarifa ya kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

Mhe. Sharifu A. Samwel alieleza kuwa Halmashauri ilikuwa imejipanga kutengeneza barabara km 20 katika kila kata na hadi sasa robo ya pili imekwisha na utengenezaji wa barabara haujafanyika, alitaka kujua ni lini utekelezaji wa bajeti iliyokuwa imepangwa kwa ajili ya kutengeneza km 20 za barabara katika kila kata utaanza.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ni kutoka katika mapato ya ndani na katika kikao kilichopita makubaliano yalikuwa fedha zitakazokuwa zinapatikana zitaanza kutengeneza barabara aliongeza kuwa kiasi cha fedha Tsh. 90,000,000.00 kilichotengwa hakitoshelezi kutengeneza km 20 kwa kila kata.

Mhe. Sharifu A. Samwel alitaka kujua kiasi cha bajeti Tsh. 90,000,000.00 zilizokuwa zimetengwa kama hazitoshi Halmashauri imejipanga vipi katika kutumia fedha hizo. Aidha aliongeza kuwa fedha hizo zisianze kufanyakazi na kuona kazi itafanyika kwa kiasi gani.

Mhe. Emmanuel N. Makashi alieleza kuwa lengo la kununua mitambo (Grader) ilikuwa ni kutengeneza barabara za Halmashauri na si kwa ajili ya kukodisha hivyo alieleza ni vyema lengo la ununuzi likaanza kutekelezwa kwanza.

Mwenyekiti alieleza kuwa barabara za Halmashauri zinatakiwa kutengenezwa na hasa kwa kuzingatia lengo la ununuzi wa mitambo ilikuwa ni kutengeneza barabara za Halmashauri na si kukodisha mitambo hiyo, hivyo alisema ni vyema utengenezaji wa barabara ukaanza maramoja.

Mhe. Felister N. Kabasa alishauri kuwa katika utengenezaji wa barabara ni vyema barabara ziwe zinatengenezwa kipindi ambacho ardhi bado inakuwa na unyevunyevu ili barabara ziwezekuwa imara zaidi.

Elimu, Afya na Maji

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.Doa M. Limbu aliwasilisha taarifa ya kamati yake, taarifa ya kamati yake ilihusisha masuala yafuatayo:

Kuhusu mikopo inayotolewa kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana.

Ilielezwa kuwa elimu na hamasa ya taratibu za mikopo na usajili wa vikundi imetolewa katika kata 12 na zoezi bado linaendelea.

Kuhusu kufunga pampu katika kisima cha maji kilichopo kijiji cha Bugomba B

Ilielezwa kuwa pampu ya mkono aina ya TANIRA imenunuliwa na kukabidhiwa kwa Mtendaji wa Kata ya Ulewe tarehe 24/12/2016. Utaratibu kwa ajili ya kufyatua pete unaendelea na kisima hicho kitakuwa kimekamilika ifikapo Machi 31, 2017

MIKAKATI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NA MSINGI

Afisa Elimu Msingi (W) aliwasilisha taarifa hiyo ikionesha idadi ya wanafunzi na miundombinu iliyopo na upungufu kwa kila shule kisha alieleza mikakti inayoweza kufanikisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na kuondokana na upungufu uliopo kwa idara za elimu msingi na sekondari kama ifuatavyo:

1. Halmashauri kupitia vyanzo vya mapato ya ndani itenge fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwenye shule zenye maboma kwa kuanza na zile zenye uhitaji mkubwa Zaidi
2. Idara ya Elimu Sekondari imetenga bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu katika shule mpya za sekondari Ubagwe, Bukomela na Mapamba ili ziweze kusajiliwa hivyo kupunguza mrundikano wa wanafunzi katika baadhi ya shule jirani
3. Idara ya Elimu Msingi imetenga sh.496,000,000.00 katika bajeti ya CDG mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu katika shule.
4. Kushirikisha wananchi katika ujenzi wa maboma ya vyumba vya madarasa kupitia Kamati za Shule/Bodi za Shule na Kamati za Maendeleo za Kata
5. Halmashauri kuweka katika mpango wa bajeti kujenga majengo ya utawala
6. Kuhakikisha vyumba vya madarasa vinatumika kwa malengo husika ili kupunguza uharibifu wake
7. Kuandaa andiko na kupeleka kwa wadau wa maendeleo ili waweze kusaidia kutatua changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa

Baada ya mwenyekiti kuwasilisha taarifa ya kamati ya Elimu, Afya na Maji, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

Mhe. Pili E. Sonje alieleza kuwa wananchi walihamasishwa kujenga maeneo ya kuhifadhia magari ya wagonjwa (Ambulance car parking) lakini magari hayo hayapatikani katika vituo vya afya alishauri suala hilo lizingatiwe.

Aidha alipongeza kwa baadhi ya shule zilizofanya vizuri katika matokeo ya mtihani kidato cha nne.

Mhe. Paschal N. Mayengo alieleza kuwa kuna kisima kilichimbwa katika kijiji cha kangeme lakini bahati mbaya maji yale yalikuwa na chumvi ilikubaliwa kuwa kitachimbwa kisima kingine kwani chanzo cha fedha ilikuwa ni fedha za wafadhili.

Pia alitaka kujua Halmashauri ina mpango gani wa kukamilisha nyumba ya muuguzi katika zahanati ya ulowa ili kuwezesha kina mama wanapokuja kujifungua wapate huduma stahiki.

Vilevile alishauri ujengwe uzio katika hostel ya wasichana shule ya sekondari ulowa ili kuwezezesha wanafunzi wa kike kupata elimu katika mazingira salama.

Kaimu Mhandisi wa maji alieleza kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 kata ya Ulowa Kangeme imetengewa bajeti kwa ajili ya uchimbaji wa kisima. Aidha aliongeza kuwa isingekuwa tatizo la maji ya chumvi kisima cha maji kingekuwa kimeshapatikana katika kata ya Ulowa na kingekuwa kimekamilika.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa Halmashauri ina magari matatu na yanafanya kazi eneo lote la Halmashauri iwapo gari moja litakuwa bovu Halmashauri huyaweka magari hayo kuwa eneo la Halmashauri ili linapohitajika liweze kufika mahala stahiki kwa wakati.

Kuhusu uzio wa hosteli ya Ulowa alisema kuwa mwandisi wa Ujenzi (W) atatembelea shule hiyo na maamuzi yatafanyika.

Mhe. Yohana E. Mange alisema kuhusu michezo katika kitengo cha utamaduni kuwa tarehe 08/03/2017 ni siku ya wanawake Duniani hivyo kama kutakuwa na uwezekano siku hiyo kuwe na michezo kati ya waheshimiwa madiwani na wataalam.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa Halmashauri tayari imefanya maandalizi ya siku ya tarehe 08/03/2017 alisema shughuli zifuatazo zitafanyika:-

i) Uchangiaji wa ujenzi wa hosteli sekondari ya kisuke.
ii) Uchangiaji wa damu kwa hiari hususani kuwasaidia akina mama wajawazito pindi wanapojifungua.
iii) Kuhimiza wananchi kujiunga na mfuko wa CHF iliyoboreshwa hasa kinamama.

Aidha aliongeza kuwa kuhusu mechi kati ya waheshimiwa madiwani na wataalamu wataangalia kama uwezekano huo utakuwepo.

Mhe. Mkomba P. Daudi alieleza kuwa mradi wa maji wa Iboja hauendelei na Baadhi ya kazi zimetajwa kufanyika lakini haziendelei hivyo alitaka kujua mradi huo utakamilika lini. Pia alitaka kujua mradi wa maji ya ziwa viktoria utafika lini eneo la Halmashauri.

Mwenyekiti alieleza kuwa mpango wa maji ya ziwa viktoria utafika katika kata sita (6) na vijiji vyote ambavyo viko ndani ya km 12.

Mhe. Damas J. Njige alieleza kuwa katika utoaji wa mikopo kwa vikundi vya ujasiliamali mikopo itolewe kwa kuzingatia uwiano katika kata zote.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa fedha bado zinaendelea kutolewa kwa wajasiliamali na muda wa karibuni Halmashauri imetoa kiasi cha Tsh. 30,000,000.00 ambayo bado iko benki kwenye mchakato kwa ajili ya mgawanyo na fedha hizo zitagusa vikundi kwa kata zote ishirini (20).

D) KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO

Makamu Mwenyekiti Mhe. Gagi Lala Gagi aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwa niaba ya Mwenyekiti. Taarifa ilihusisha taarifa ya mapato na matumizi, vikao ambavyo viliketi katika kipindi cha robo ya pili (Oktoba – Desemba) 2016/2017 na mihtasari yake ilithibitishwa:

Kuhusu majengo ya Halmashauri ya Ushetu yaliyopo mjini Kahama

Ilielezwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ina jumla ya majengo kumi na nane (18) ikiwa majengo matano (5) yalitumika kwa makazi ya watumishi, majengo mawili (2) yalikuwa maghala ya kuhifadhia vifaa vya Halmashauri, majengo kumi (10) yalikuwa yanatumika kwa shughuli za kiofisi na jengo moja (1) lilitumika kwa shughuli za mikutano. Majengo mengi yanahitaji ukarabati wa kawaida kama kupaka rangi, kurekebisha mfumo wa umeme, kukarabati vyoo, sakafu katika majengo 14 na ukarabati wa madirisha na milango.

Kamati haikufanikiwa kupata nyaraka zozote za hati miliki ikiwa ni pamoja na majengo ya nyumba za watumishi wa halmashauri na jengo la ofisi ya mganga mkuu ingawa majengo hayo yote yameshapimwa na kupewa ploti namba.

Kamati ilishauri aina ya uwekezaji utakaofaa katika majengo hayo kama ifuatavyo;

i. Kupangisha majengo yote kwa Taasisi, Shirika, Kampuni inayojishughulisha na utoaji huduma au shughuli zisizoweza kuathiri muundo wa majengo na mazingira ya maeneo yalipo majengo hayo.
ii. Kupangisha jengo moja moja kwa watu binafsi, kampuni, Taasisi na mashirika

iii. Shughuli zinazoweza kuruhusiwa niuendeshaji wa hotel,kiofisi, mafunzo na utunzaji wa vifaa, na hakutakuwepo na ruhusa ya kubadili muundo wa majengo.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walisisitiza kuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji ihakikishe inatunza mihtasari ya mgawanyo wa rasilimali kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Kahama Mji pamoja na ile ya mgawanyo wa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu na Msalala.

Kuhusu utozaji wa ushuru wa (Hotel levy)
Ilielezwa kuwa, Halmashauri katika zoezi la kuzitambua nyumba za kulala wageni katika kata zote 20 lilifanikiwa, na kubaini kuwa kata 14 tu ndizo zenye nyumba za kulala wageni. Jumla ya nyumba za kulala wageni 40 zimebainishwa na zinauwezo wa kukusanya wastani wa Tsh.269,820,000.00 kwa mwaka kulingana na bei zinazotozwa kwa kila chumba.Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu yaweza kupata Tsh.26,982,000 (10% ya mapato ya nyumba za kulala wageni) kwa mwaka.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, wajumbe walikubaliana kwa pamoja kuwa itozwe 10% ya mapato kwa kila nyumba ya kulala wageni.

Kuhusu kitabu cha kukusanyia mapato kilichopotea katika kizuizi/geti la mpunze.

Ilielezwa kuwa, suala hilo bado lipo kwenye uchunguzi wa polisi, mara uchunguzi utakapokamilika, taarifa kamili itawasilishwa.

Wajumbe walishauri kuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) ifuatilie suala hilo ili kuweza kupata majibu.

Barua ya kukabidhi majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu yaliyopo mjini Kahama

Ilielezwa kuwa Halmashauri ilipokea barua kutoka Halmashauri ya Mji Kahama yenye Kumb.NA.KTC/CO.10/2/2 ya tarehe 19/09/2016 iliyokuwa ikiitaka Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kukabidhi majengo waliyokuwa wanatumia kama ofisi mjini Kahama kwa madai kuwa ni mali ya Halmashauri ya Mji Kahama.

Katika kujibu barua hiyo, Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kwamba;

- Halmashauri ya wilaya ya kahama iligawanywa na kupatikana halmashauri mbili, yaani Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na Halmashauri ya Mji Kahama Julai, 2012, wakati huo Halmashauri ya Ushetu haikuwepo. Kwahiyo si haki kuelekeza madai hayo kwa Halmashauri ya Ushetu.

- Wakati Halmashauri ya Mji- Kahama inaanzishwa Julai, 2012 waraka wenye Kumb. Na.2HB.215/355/01 wa tarehe 14/12/2012, uliorejea katika barua hiyo, haukuwapo. Hivyo waraka huo sio sahihi kuutumia kwa marejeo na kwa matakwa hayo.

- Kwamba barua Kumb.Na. UDC.S.20/09/41 ya tarehe 24/03/2014 iliyotumwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuwa majengo ya Halmashauri ya Ushetu yaliyopo Kahama- Mjini ni mali ya Halmashauri ya Mji Kahama ni barua batili kwa kuwa haikutelekeza maamuzi ya kikao chochote cha Baraza la Madiwani, ambacho ni kikao chenye maamuzi ya mwisho juu ya mali za Halmashauri, nabarua hiyo haikuomba kubadilisha umiliki wa majengo ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu. Pia barua hiyo haikuhusu wala haikuzungumzia mgawanyo halali wa mali kati ya Halmashauri ya wilaya ya Ushetu na Halmashauri ya Kahama Mji, kwa hiyo si sahihi kuirejea kwa makusudi yao.

- Kwamba hakuna maamuzi yoyote yanayofanywa juu ya mali za Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu bila ridhaa ya vikao vyenye mamlaka hiyo.

- Hivyo ili takwa lao litekelezwe, ni lazima kuwasilisha barua hiyo kwa mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa maamuzi halali na majibu ya maamuzi hayo ndiyo yatajibu barua hiyo.

Wajumbe wote waliunga mkono majibu ya barua ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ushetu yenye Kumb.Na.UDC/CA.10/03/09 ya terehe 20/10/2016 na kusisitiza mihtasari ya vikao vya mgawanyo itatumiwa kama rejea. Halmashauri ya wilaya ya Ushetu haioni sababu za kutoa majengo hayo kwa Halmashauri ya Kahama Mji kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu haikugawana mali na Halmashauri ya Kahama Mji.

Ilielezwa kuwa Katika mgawanyo wa Halmashauri rasilimali zote za Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ziligawanywa ikiwa ni watumishi, majengo, madeni, vitendea kazi na magari. Hivyo pamoja na Halmashauri ya Ushetu kuhamia makao makuu yake ya Nyamilangano ina changamoto kubwa ya miundo mbinu kama umeme, mawasiliano, mfumo wa “epicor” na “Lawson” hivyo kuna baadhi ya kazi hufanyika kwenye majengo hayo yaliyopo mjini Kahama.

Mapendekezo ya ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato mwaka 2016/2017 kuanzia Januari, 2017

Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu hukusanya mapato ya ndani kwa kutumia vyanzo vya mapato vilivyoainishwa kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017, kama vile minada, magulio ushuru mbalimbali wa kilimo na misitu ambavyo hukusanywa kwa kutumia mageti.

Kutokana na changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia watendaji wa kata, vijiji na migambo, gharama za ukusanyaji na ufuatiliaji zimekuwa kubwa kuliko matarajio ya Halmashauri.

Ilishauriwa kuwa, vyanzo hivyo vibinafsishwe na ubinafsishaji uanze mwezi januari 2017 kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 kwa kipindi cha miezi sita tu (kuanzia Januari 2017 hadi Juni 2017) ili kuwezesha Halmashauri kuweza kupima ukusanyaji kwa kutumia wazabuni na watendaji.

Wajumbe kwa pamoja waliunga mkono hoja ya mapendekezo ya ubinafsishaji wa vyanzo vya mapato mwaka 2016/2017 kuanzia Januari, 2017 hadi Juni 2017.

Mabadiliko ya mradi kupitia mfuko wa barabara

Ilielezwa kuwa taarifa hiyo ililenga kupata kibali cha kufanya mabadiliko ya jina la mradi kutoka mradi wa barabara ya Uyogo – Ushetu- Ulowa (kipande cha Uyogo- Ushetu km 7) kuwa Nyamilangano- Butibu, Nyankende- Mwabomba na Ushetu- Muhuge. Hii ni kutokana na kuhitajika kuweka makalvati mita 14, kuweka moramu katika tuta barabara za Nyamilangano-Butibu lenye udongo mweusi kwa gharama ya shilingi milion 24.7 na kunyanyua tuta la barabara ya Mwabomba – Nyankende, kumwaga changarawe na kujenga makalvati mita 14 kwa gharama ya shilingi milion 39.1.Pia kukarabati barabara ya Ushetu-Muhuge kwa gharama ya shilingi milioni 46 ili barabara hizo ziweze kupitika muda wote.

Gharama za mradi huu zimetokana na fedha za bajeti ya mwaka 2013/2014 baada ya kusimama kwa mradi wa Uyogo- Ulowa kutokana na Mkandarasi kufutiwa mkataba kwa kazi iliyokuwa hairidhishi na muda wake wa kimkataba kuisha na kushauri matengenezo haya kuingizwa kwa barabara za Bulungwa-Ulewe (eneo korofi) na Bugomba –Nyalwelwe (eneo korofi) kupitia Mfuko wa Barabara kwa bajeti ya mwaka 2016/2017.

Wajumbe waliridhia kwa pamoja kuwa barabara hizo zifanyiwe ukarabati wa haraka ili ziweze kupitika muda wote hasa katika msimu wa mvua.

Taarifa za kiutumishi na mashauri ya nidhamu

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa mwezi Oktoba na Novemba 2016, Iliandaa taarifa za kiutumishi kama ifuatavyo;

- Watumishi waliostaafu kazi kwa mujibu wa sheria au hiari 1
- Watumishi waliofukuzwa kazi 2
- Watumishi walioacha kazi 1
- Watumishi waliopewa barua za onyo 12
- Watumishi wenye mashauri ya kinidhamu 18
- Watumishi wenye kesi mahakamani 1

Halmashauri ilifanikiwa kulipa mishahara kwa kiasi cha Tsh 1,127,808,850. Watumishi 1852 kwa gharama ya Tsh 1,122,425,500/= kwa ruzuku toka serikali kuu na watumishi 22 kwa gharama ya Tsh 5,383,530 wanaolipwa mishahara yao kwa ruzuku ya mapato ya ndani, kati yao ni watumishi 18 wa mkataba na watumishi 04 wa ajira ya kudumu. Pia alieleza kuwa kuna mazoezi mawili ya Kitaifa yamefanyika ambayo ni ujazaji wa fomu,

upigaji wa picha na alama za vidole kwa ajili ya maombi ya vitambulisho vya Uraia (NIDA) na Zoezi la uhakiki wa vyeti vya watumishi.

Taarifa ya matokeo ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi (PSLE) 2016/2017

Halmashauri ilikuwa na jumla ya watahiniwa waliosajiliwa 3503 (Wavulana 1671 na Wasichana 1832). Mtihani ulifanyika katika vituo 98 (shule za msingi).
Baraza la Mitihani la Tanzania lilitangaza rasmi Matokeo ya Mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2016 tarehe 28/11/2016 ambapo jumla ya wanafunzi 2093 (Wavulana 1096 Wasichana 997) walichaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu Sekondari 2017 kwa mchanganuo ufuatao

Ilielezwa kuwa waliojiunga shule za kutwa (shule za kata) ni 2080 Wav 1087 na Was 993) na waliojiunga shule za bweni ni 13 (Wavulana 9 na Wasichana 4).

Matokeo ya Mtihani wa kuhitimu elimu ya msingimwaka 2014-2016

NA	MWAKA	WALIOSAJILIWA			WALIOFANYA			WALIOFAULU			ASILIMIA
		WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML	
1.	2014	1962	2235	4197	1893	2172	4065	1076	840	1916	47.17
2.	2015	1718	1997	3715	1695	1952	3647	1118	971	2089	57.28
3.	2016	1671	1832	3503	1653	1822	3475	1096	997	2093	60.23

Baada ya taarifa ya kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kuwasilishwa, wajumbe walijadili kama ifuatavyo:

Mhe. Pili E. Sonje alishauri Idara ya Utumishi ni vyema wakati wa kupandisha madaraja kwa watumishi iandae taarifa sahihi za watumishi ambao bado hawajapandishwa madaraja na wanaotakiwa kupandishwa daraja kwani kuna watumishi ambao hawajapandishwa madaraja zaidi ya miaka saba.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa ushauri huo umechukuliwa, kuhusiana na watumishi kupandishwa daraja kuna taratibu mbalimbali zinazokuwa zinafuatwa ili mtumishi kuweza kupandishwa daraja ikiwa ni pamoja na upimaji shirikishi wa utendaji kazi (OPRAS).

Mwenyekiti alieleza kuwa masuala ya watumishi yasimamiwe kwa kuzingatia haki na misingi ya kisheria.

Mhe. Esther M. Imambo alishauri Halmashauri kufanya manunuzi yake kwa bei halisi hasa kuhusiana na matengenezo ya gari la kubebea wagonjwa namba 9804 kuwa gharama zilizotumika Sh. 11,040,316.00 katika matengenezo ni kiasi kikubwa kwa kutengeneza gari moja hivyo ni vyema wakati wa matengenezo kuangalia wazabuni ambao wanaweza kufanya kazi kwa gharama nafuu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) alieleza kuwa matengenezo ya gari namba 9804 mara ya kwanza ilipelekwa TAMESA na gharama yake ilikuwa takribani sh.milioni 16 lakini lilipopelekwa kwa wazabuni wengine gharama ilipungua.

Mheshimiwa Makashi alieleza kuwa kuna watendaji wa vijiji ambao wanakaimu vijiji zaidi ya kimoja na wanatoka mbali zaidi na makazi yao hali inayopelekea kushindwa kusimamia vyema majukumu yao ya ulinzi na usalama hasa yanapotokea matukio mbalimbali vijijini au katani.

Aidha alieleza kuwa Ofisi ya kijiji cha Sabasabini imefungwa zaidi ya miezi miwili iliyopita na haijafunguliwa, alisema kuwa suala hilo ni ukiukwaji wa sheria na haki za binadamu kwani wananchi walichangia fedha pamoja na nguvu zao katika ujenzi wa ofisi hiyo.

Pia kuna fedha za mradi wa ujenzi wa ukamilishaji wa maabara kiasi cha Tsh. 10,000,000.00 kilitolewa lakini tatizo linalo kwamisha utekelezaji wa kazi hiyo kuanza ni BoQ kwani hadi sasa haijakamilika hali inayopelekea kushindwa kuonesha taarifa ya utekelezaji wa mradi katika robo ya tatu.

Aidha aliongea kuhusu uchimbaji wa kisima kirefu cha maji Sabasabini, alitaka kujua mradi huo ni lini utekelezaji wake utaanza.

Mwenyekiti alieleza kuwa kuhusu BoQ ilishaelekezwa kuwa maeneo husika yenye miradi ya maendeleo Diwani wa kata husika apewe nakala ya BoQ.

Kaimu Afisa Utumishi (W) alieleza kuwa mnamo tarehe 24/01/2017 alifanya ziara kwa baadhi ya kata ikiwa ni pamoja na kata ya sabasabini, Kuhusu kufunga Ofisi alifafanua kuwa alikuta kaimu Mtendaji akifanya kazi kwa mkataba wa serikali ya kijiji huku akiendelea kutumia nyaraka za serikali wakati ajira hizo zilisitishwa tangu 01/07/2016.

Mwenyekiti alishauri kuwa Mhe. Elias J. Kwandikwa (MB) asaidie kupata Ikama ya watendaji wa vijiji kama ilivyokasimiwa kwenye bajeti ya 2016/2017 na 2017/2018 mara tu ajira hizo zitapo anza.

Mhe. Doa M. Limbu alieleza kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji ya visima virefu na vifupi kuwa kila mwaka bajeti inawasilishwa lakini fedha hailetwi hivyo alishauri katika miradi hiyo utafiti wa maji uanze na pindi fedha itakapopatikana kazi itaendelea.

Mhe. Elias J. Kwandikwa (MB) alifafanua kuwa hatua za awali za utekelezaji wa miradi ya maji zianze, alieleza kuwa katika utekelezaji wa miradi ya maji Mhandisi wa maji (W) anatakiwa kutafuta mkandarasi na kuanza utaratibu wa kufanya utafiti wa maji, pindi anapopata Hati ya madai ya malipo kwa kazi zilizofanyika “certificate” itawasilishwa katika

wizara husika ili mradi huo kuanza kulipwa vinginevyo miradi itakuwa inaishia kwenye mpango wa bajeti.

MUHT.NA.BM/50/2016/2017 – KUFUNGA MKUTANO

Kuhusu timu ya mpira wa miguu ya Euro - City kutoka kata ya Ulowa

- Uongozi wa timu hiyo walikaribishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani wakiwa na kombe la ushindi katika michuano iliyofanywa na timu kuibuka washindi watakaowakilisha wilaya ya Kahama katika ngazi ya mkoa.
- Afisa Utamaduni (W) alitaja kiasi cha Tsh. 425,000/= ambacho kimechangwa na waheshimiwa madiwani pamoja na wataalam katika kuifadhili timu hiyo.
- Mwenyekiti wa kamati ya EAM aliwapongeza wachezaji na uongozi wa timu ya Euro – City kutoka Ulowa kwa ushindi na kuongeza kuwa timu hiyo ndiyo imekuwa kikundi cha kwanza cha kijamii kutembelea na kufika katika mkutano wa Baraza la madiwani la Halmashauri ya wilaya ya Ushetu.

Aidha alikabidhi jumla ya Tsh. 425,000/= ambazo zilichangwa na madiwani na wataalam waliohudhuria mkutano huo.

- Msemaji wa Timu hiyo Ndugu Philip Chimi alishukuru kwa ufadhili uliotolewa na kuomba waheshimiwa madiwani kusaidia, kuomba ufadhili kwa wadau mbalimbali ili wasaidie kuiwezesha timu hiyo. Hii ni pamoja na Halmashauri kusaidia kufadhili timu hiyo.
- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa amepokea maombi ya ufadhili kutoka timu ya Euro – City na atayafanyia kazi na kutoa mrejesho kwa timu hiyo.

Mambo aliyozungumzia afisa serikali za mitaa

Katibu serikali za mitaa aliongea kwa niaba ya Katibu Tawala (M) kuhusu suala la watumishi kupandishwa daraja alieleza kuwa wakuu wote wa Idara wanatakiwa kushirikiana na Afisa Utumishi (W) kwa kupeleka mapendekezo ya majina ya watumishi wanaotakiwa kupandishwa madaraja na kasha idara ya utawala utumishi wataandaa ikama kwa kuzingatia miongozo iliyopo na kupeleka suala hili kwa bodi ya ajira.

Kuhusu ufugaji wa samaki alieleza kuwa kuna kituo cha ufugaji wa samaki wilaya ya Igunga ambapo wataalamu, madiwani na wananchi wanaweza kwenda kujifunza (Best practices) na kuona jinsi mayai ya samaki yanavyototolewa, vifaranga wanavyokuza, nyavu za kuvulia samaki zinakuwa na kipimo gani na hata jinsi ya kuweza kuzuia wanyama hatari kama kenge na wengineo.

Katibu alimkaribisha mwenyekiti kwa ajili ya kufunga mkutano.

Mwenyekiti alieleza kuwa maazimio na maamuzi yanatolewa katika vikao ni vyema yakaandikwe vizuri na kutekelezwa mapema na hivyo taarifa hizo zisiishie kwenye maandishi tu bali utekelezaji unatakiwa kufanyika.

Aidha alieleza kuhusu hali ya hewa kuwa kwa ujumla si nzuri hivyo ni vyema maafisa kilimo wakatoa elimu kwa wananchi kulingana na mvua inayonyesha wananchi walime mazao yanayoendana na hali ya mvua iliyopo kama kilimo cha viazi na mtama kulingana na mbegu ya zao hilo kadri zilivyopatikana.

Mwenyekiti alifunga kikao saa 08:44 mchana.

MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA

NA

…… …… ……

Ndg. Sadick J. Mwita **Mhe. Juma A. Kimisha**

KATIBU **TAREHE** **MWENYEKITI**